



# Kupangiya Makuta

Maisha ya Amerika inakuwaka beyi wakati ingine. Utumikishe makuta yako muzuri, alafu usiingiye mu ma deni za kukupita kipimo. Wa raiya wa Amerika bengi banachunga makuta yabo mu banki kwa sababu makuta ikiwa mu Banki ni kama inachungwa na serkali ya Amerika. Nikusema hizo makuta zikipoteya ao zikiibiwa humo mu banki serkali ya Amerika itazilipa. Ni lazima ujifunze namna ya kutumikisha banki kupitiya machine, ujifunze kuhusu crédit, deni, kupangiya makuta na kulipa ma taxes.

## KUTUMIKISHA BANKI

Banki zinasaidiya mu njiya za mingi sawa kufungula compte ya kuwekeya amo makuta. Ukifunguwa **compte ya ma chèques**, itakuruhusu uuze kitu yoyote unataka ukitumikisha chèque, ao carte ya hiyo compte, ao ukilipa kupitiya internet. Haupashwe kutumikisha Zaidi ya makuta yenyi kuwa ndani ya compte yako. Ukitumikisha zaidi ya makuta yenyi kuwa ndani ya compte yako banki itakulipisha makuta Fulani kama malipizi.

**Compte ya kuweka akiba (compte d'épargne)** ni compte ya kukusaidiya kuchunga makuta kwa sababu unapenda uzitumikishe nyuma ya myezi ao myaka mingi. Hata hivyo unaweza kukamata hizo pesa wakati yoyote, alakini unapashwa enda ku banki banakupa azo ku mkono ao unatumikisha carte ku machine ya makuta. Comptes hizo za kuwekeya ndani makuta zinakuwaka na kanuni fulani, inawezekana bakuambiye kama makuta fulani zinapashwa kuwa ndani ya compte wakati yoyote ao banaweza kuambiya makuta ngapi unaweza kamata kwa siku.

## CRÉDIT NA DENI

Kuko namna mingi zakuomba deni hapa Amerika. Yenyi batu banafanya zaidi ni kuomba carte ya crédit, alakini hiyo carte inaweza kukuruhusu kukamata deni ya makuta kidogo tu, na utakuwa na muda mufupi ya kulipa deni hiyo bila faida. Kama ni deni ya makuta mingi njo unataka, sawa kuuza gari ya mupya, waamerika wengi banaomba moja kwa moja banki ibakopeshe.

KUPANGIYA MAKUTA








Kuna bitu mingi unapashwa juwa mbele yakukopesha makuta. Ukikopesha makuta kidogo na unalipa haraka hiyo deni, utajulikana kama mutu mwenyi analipaka ma deni zake kwepesi. Benyi kukukopesha batajulishwa kama unalipaka ma deni zako ao hapana kutokeya ma fasi ulikopeshaka mu myezi na myaka iliyopita, njo bajuwe kama kukukopesha ni hatari ao hapana. Wakipashwa habari muzuri ya kusema kama unalipaka ma deni zako, alafu itakuwa kwepesi ukopeshwe makuta yakuuza kitu kama gari.




Sasa, ikiwa haulipake deni zako kwa wakati, unaweza shtakiwa. Piya, unapashwa lipa ma faida za hizo deni na hiyo inaongeza makuta zenyi unapashwa lipa.

## CARTE YA DENI NA CARTE YA KAWAIDA

Carte ya kawaida na carte ya deni binafananaka karibu, alakini kuna tafauti ya mkubwa. Unaweza zitumikisha zote kwa kuuza bitu wakati unaenda fasi ya kuuziya ao kuuziya ku internet, alakini carte ya kawaida inakuruhusu kukamata makuta mu compte yako ya hakiba (compte d'épargne) ao mu compte yako unatumikishaka kwa kupokeya makuta zako.

## DENI YA MAKUTA YENYI ILIKUSAFIRISHA

Bakimbizi banaruhusiwa kupewa deni ya kulipa safari yabo kuenda Amerika na hiyo deni watailipa bila kuongeza faida juu. Kwa kupewa hiyo deni, banakulomba u signer baruwa yenyi kusema kama unahakisha kama utalipa hiyo deni tokeya utafika na utamaliza illipa nyuma ya myezi 46. Utapata facture ya kwanza mu myezi sita yakufika Amerika, yenyi kukuomba ukuwe nalipa deni yako ya safari ukilipa makuta kidogo kidogo kila mwisho wa mwezi na hiyo ni ni deni ya kwanza yenyi itaonesha kama uko mwepesi kulipa deni. Ikiwa uko na shida yoyote kwa kulipa, uambiye ofisi ya kuhamishwa (Bureau de Réinstallation).

## KUPANGIYA MAKUTA YAKO

Ni mzigo wako kujuwa ginsi ya kutumikisha makuta yako, alakini batumishi ya shirika ya kuhamishwa (agence de réinstallation) banaweza kukusaidiya kupangiya makuta yako. Mpango wa makuta ni kujuwa makuta ngapi uko nazo, ngapi unaweza tumikisha, na ngapi unaweza weka.




## FAIDA NI KUSEMA NINI?

Faida ni makuta unapashwa ongeza yulu ya makuta ulikopeshwa kwa huyo mutu mwenyi alikukopesha kwa sababu alikuona kama mutu wa maana. Wakati unakamata deni (kupitiya carte ya crédit ao kupitiya banki), utalipa faida. Deni ya kulipa nyuma ya muda kidogo inakuwaka na faida kubwa yakulipa deni kubwa yenyi kupewa na banki. Kufanya hesabu ya kujuwa ni faida yapata gani utalipa ku deni fulani ni mafikiri ya lazima na itakusaidia ndani ya mpango ya kulipa deni na unapashwa kuuliza wakati yote unakamata deni.

Wakati unaweka makuta yako ndani ya compte yako ku banki zitaongezeka ako faida kwa sababu banki inatumikisha makuta yako kukopesha batu bengine. Kuna banki zenyi kupana faida ya mingi, alakini hizo banki zinaweza kutiya mpaka ku pesa ngapi unaweza chukuwa kwa siku piya zinaweza kukatiya muda yenyi hauwezi chukuwa makuta.

Utakuwa na lazima ya kuuza kila mwezi byenyi uko nabyo lazima na bingine. Ikiwa uko na mafikiri ya kufanya bingine mu myaka yenyi kuwa mbele, sawa ginsi kuuza nyumba, wakati utakuwa ulisha uza byako bya mu nyumba, unaweza kuwa unaweka mu compte ya hakiba (épargne) kila mwezi.

## KULIPA MA TAXES

Makuta za taxes, hapa Amerika, zinasaidiya kufanya kazi za kusaidiya wakaaji, piya na bakimbizi. Makuta ya taxes njo inalipa masomo, njo inatengenezesha ma barabara na hizo barabara za autoroutes; kulipa kazi ya police, kazi ya ba pompiers, kulipa kazi za ambulances; piya kulipiya kazi za kusaidiya ma jamaa (programmes des services sociaux)

Batu benyi kuishi hapa Amerika banalipa taxes tatu tafauti:

- **Taxes zenyi banakamata ku makutu zenyi ulipokeya.** Kila mutu mwenyi kutumika analipa hizo taxes za serkali ya Amerika. Hizo taxes ni kazi kwenyi unatumika njo banazikamataka ku mshahara yako banazilipa serkali.
- **Taxes zenyi kuangaliya nyumba ao bulongo ya mutu.** Serkali ya muji (administration locale) banaweza omba taxes za nyumba, za bulongo, na ma nyumba zako. Mwenyi nyumba analipa hizo taxes ju ya nyumba kwenyi unalipiya. Serkali zingine za muji (administration locale) zinalipisha taxes za mitugari.
- **Taxes unayolipa ukiuza kitu.** Mu inchi mingi za Amerika, batu banalipaka makuta ya taxes wakati banauza bitu fulani. Taxe hiyo wanaiongeza ku makuta yenyi ulitowa kwa kuuza kitu. Mu ma inchi zigine za Amerika, habalipishe taxes ku bitu bingine sawa chakula ao dawa. Ku bitu bingine sawa, tumbagu ao pombe, malipo ya taxe inaweza kuwa yulu zaidi.

**Cultural Orientation Resource Exchange**
8719 Colesville Road, 3rd Floor • Silver Spring, MD 20910
For more information, visit the CORE Resettlement Navigator website at **corenav.org**.

Cultural Orientation Resource Exchange

The contents of this fact sheet were developed under an agreement financed by the Bureau of Population, Refugees, and Migration, United States Department of State, but do not necessarily represent the policy of that agency and should not assume endorsement by the Federal Government. **This material is in the public domain and may be reproduced.**